

JOHARI ZARI,
S.L.P. 1252,
JIIMARISHE.

MEI 8, 2024.

MKURUGENZI MKUU, KIWANDA CHA NADHIFU,
S.L.P. 67980,
MAFANIKIO.

Kwa Bwana/Bibi,

MINT: OMBI LA NAFASI YA KAZI

Ninachukua fursa hii kutuma ombi la kazi ya ushonaji katika kiwanda chako cha Nadhifu. Baada ya kusoma tangazo la nafasi ya kazi katika gazeti la Baraza, tarehe sita Mei, mwaka huu, nimeamua kutuma ombi langu.

Mimi nina umri wa miaka kumi na minane. Nilihitemu masomo yangu ya Gredi ya Kumi na Mbili katika shule ya Elimubora mjini Jitegemee. Nilikuwa nikisoma kwa bidii nikiwa na matarajio ya kufanikiwa maishani. Bila shaka, mimi ni mtu mwenye kujituma na kuwajibika.

Tangu nilipokuwa mdogo, nilikuwa na azma ya kuwa mshonaji. Nilipokuwa shuleni, nilikuwa nikishiriki katika mashindano ya ushonaji kila mwaka. Kwa miaka mitatu mtawalia, nilifanikiwa kushiriki katika kiwango cha kitaifa. Niligundua kuwa nina kipawa cha ushonaji na nikaahidi kuendelea kukikuza nikipata fursa. Kwa hivyo, nilipoona tangazo la nafasi ya kazi katika kiwanda chako, nilijua kwamba nitapata fursa ya kutimiza ndoto yangu.

Iwapo utanipa fursa hii, ninaahidi kwamba nitatia bidii katika kazi yangu. Nitahakikisha kwamba ninafanya kila niwezalo kufikia mataraji yako. Nitafurahi kufuata sheria na kanuni zote za kiwanda chako. Pia, ninaamini kwamba kazi nitakayofanya zitaboresha uwezo nilio nao.

Kwa maelezo zaidi kuhusu wasifu wangu, tafadhali rejelea wasifukazi ambao niambatananisha na barua hii.

Ninatarajia kwamba utazingatia ombi langu. Asante sana kwa muda wako.

Wako mtiifu,



Johari Zari